TANGAZO LA SERIKALI Na. 672 La Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI ZA MWAKA 2020

Jina

Tangazo la Serikali Na. 274 la Mwaka 2011

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Missenyi za Mwaka 2020 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za Mwaka 2011 ambazo katika Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 4

2. Kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo kuu kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka kifungu kidogo kifuatacho;

"(2)Halmashauri itatoza ushuru wa magari ya abiria na mizigo kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi".

*Tangazo la Serikali Na. 672 (Inaendelea.)*

Kufutwa na kuwekwa upya kifungu cha 12.

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta Kifungu cha 12 na badala yake kuweka kifungu kipya kifuatacho;

Adha-bu

"12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo".

Kufu-twa na kuwekwa upya kifungu cha 13.

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 13 na badala yake kuweka kifungu kipya kifuatacho:

Kufifilisha kosa

"13. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha shilingi laki moja iwapo mkosaji atakuwa tayari kukiri kosa kwa hiari kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi".

Kufu-twa kwa Jedwali la Kwanza

5. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Kwanza na badala yake kuweka Jedwali lifuatalo;

Marekebisho ya

6. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuweka Jedwali la Pili lifuatalo:

*Tangazo la Serikali Na. 672 (Inaendelea.)*

Jedwali
la Pili.

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4 (2))*

*Ushuru wa Magari ya Abiria na Mizigo*

| Aina ya gari | Kiasi cha ushuru |
|---|---|
| 1. Basi Kubwa la Abiri 46-65…………………………… | 5,000/= kwa siku |
| 2. Basi dogo la Abiria 1-45 ……………………………… | 2,000/= kwa siku |
| 3. Gari la mizigo tani 7 na kuendelea…………………… | 10,000/= kwa siku |
| 4. Gari la mizigo chini ya tani 7………………………….. | 7,000/= kwa siku |
| 5. Gari binafsi lisilo la biashara …………………………. | 500/= kwa siku |
| 6. Taxi ………………………………………………….. | 1,000/= kwa siku |
| 7. Pikipiki…………………………………………………… | 500/= kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 13)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya……………………… ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, kuwa tarehe …………… mwezi ……………mwaka…………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za mwaka 2011.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutekeleza wajibu wangu badala ya kushtakiwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe…………… ya mwezi ……… Mwaka …………

*Tangazo la Serikali Na. 672 (Inaendelea.)*

Jina…………………………………………Saini ……………………….

Mbele ya:

Jina:…………………………………………………………………

Saini:………………………………………………………………

Cheo:…………………………………………………………….

Tarehe:……………………………………………………….....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kilichofanyika tarehe 8/11/2019 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

Projestus K. Tegamaisho
*Mwenyekiti*
*Halmashauri Ya Wilaya Ya Misenyi*

Innocent M. Mukandala
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Missenyi*

S.L

NAKUBALI

Dodoma
5 Agosti, 2020

Selemani S. Jafo (Mb),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*